Diploma Programme
Programme du diplôme
Programa del Diploma

# Swahili A: literature – Higher level – Paper 1
# Swahili A : littérature – Niveau supérieur – Épreuve 1
# Swahili A: literatura – Nivel superior – Prueba 1

Wednesday 4 May 2016 (afternoon)
Mercredi 4 mai 2016 (après-midi)
Miércoles 4 de mayo de 2016 (tarde)

2 hours / 2 heures / 2 horas

---

### Instructions to candidates

- Do not open this examination paper until instructed to do so.
- Write a literary commentary on one passage only.
- The maximum mark for this examination paper is **[20 marks]**.

### Instructions destinées aux candidats

- N’ouvrez pas cette épreuve avant d’y être autorisé(e).
- Rédigez un commentaire littéraire sur un seul des passages.
- Le nombre maximum de points pour cette épreuve d’examen est de **[20 points]**.

### Instrucciones para los alumnos

- No abra esta prueba hasta que se lo autoricen.
- Escriba un comentario literario sobre un solo pasaje.
- La puntuación máxima para esta prueba de examen es **[20 puntos]**.

2216 – 0197



© International Baccalaureate Organization 2016

International Baccalaureate
Baccalauréat International
Bachillerato Internacional

https://xtremepape.rs/

Andika uchambuzi kuhusu kifungu **kimoja** kati ya hizi:

**1.**

Florentina, mke wa Lambo! Anainua macho, anatazama hapa na pale, anatabasamu. Anainama kimya! Kisha, anatamka kwangu, akijibu kauli yangu "Mmh! Ni tatizo sana! Naliona tatizo kubwa juu ya ombi lako kwa sasa. Eh… kwa sasa nakaa na ndugu wengi. Nakaa na shemeji, mdogo wa bwanangu. Kama unavyomjua, ni mtoto mwenye akili za kikubwa na kawekwa na mume wangu kwa makusudi makubwa! Amewekwa kwa minajili ya kunichunga juu ya matendo yangu, japokuwa hayana alama hayo nitendayo. Vilivyo, mlinzi hulinda ndege washambuliao mpunga, ngano au mtama mashambani. Mke mzuri kamwe halindwi. Silaha yake kubwa ni mawazo yaliyokosa pazia. Isitoshe, naishi pia na mtoto wa shangazi, Leonila. Anasoma kidato cha nne huko Zanaki, Dar es Salaam. Msichana wa kidato hicho hapa kwetu Tanzania ni mkubwa; si vizuri kumwonyesha buyu la asali lilipo, kwani huenda akatumia utundu wake, akalionja kwa pupa. Utahatarisha maisha yake kwa kumlazimisha kuchonga zinga litakalofuga nyuki dume, ambao badala ya kutagisha asali watauma kizazi na kuleta hasara kwa umma! Watoto wa dadangu ni wakubwa vya kutosha. Kama unavyofahamu, yule asomaye darasa la saba, Nikhola, ni binti aliyekwishautoka tu ukigoli. Kuna vizingiti vingi, Mika. Kwa usalama wetu, nashauri tungeahirisha mpango huu kwa juma hili. Ukiwa tayari, unaweza kunijulisha kwa njia yoyote."

Anamaliza kunieleza baada ya kupendekeza nia yangu kwake kuwa ningekuwa tayari kuchukua nafasi ya mume wake, Lambo.

Nageuka kushoto, naketi juu ya gogo la mti huu wa *mwao*. Najishika tama, huku hatua za Florentina zikisikika cha…cha… cha ndani ya vigoma vya masikio yangu mapana. Huyoo! Anafifilia kijijini kwao, ni karibu na kijijini hapa kwetu.

Sasa natulia nayatafakari upya maneno ya Florentina. Florentina, mke wa Ofisi-Uajiri katika Shirika la Usagishaji (NMC), nimemtafuta kwa muda mrefu sasa. Kwa hakika, sikudhamiria kufanya hivyo kwa muda mrefu. Lakini tabia ya Lambo … Natulia kidogo, nashusha pumzi. Moyo wangu unadunda kwa milio mchanganyiko ya ndu…ndu…ndu… na ti… ti… kwa nguvu huku bongo langu likiwa limebeba viwazo vya msetomseto.

"Kwani lazima nije mchana, macho yakiangaza?"

"Utafanyaje?" Upande mmoja wa moyo wasaili.

"La hasha!"

"Eh?"

"Nitakuja kwa siri, ndani ya giza tiii."

Nayainua macho yangu makubwa kiasi na kuyaelekeza juu, lakini mawazo yangu nayaelekeza mwilini kwa Florentina, mwanamama ambaye bado ni tipwatipwa; lau kama keshazaa mtoto mmoja. Kizaacho si haramu, haramu kisichozaa! Mwanamama mzuri, amechanua na kuwaka mithili ya nyota. Ana mwili bojiboji … Mwangalie anavyomulika mitaani! Ana miaka kumi na sita. Umri wangu ni miaka ishirini. Nalipua mioyo ya wengi humo mitaani. Najifananisha na mumewe. Mishipa kadhaa iliyoranda mikononi mwa Ofisa-Uajiri humsaliti mbele yangu, mimi nina bado damu changa. Florentina …

Namtaka Florentina. Nina sababu kadhaa. Kwanza, nilipotafuta kazi katika Shirika hili la Usagishaji nimetendewa mengi.

"Nilitemewa mate na mesenja anayekaa mlangoni mwa ofisi ya Lambo, kwa amri ya Lambo mwenyewe."

https://xtremepape.rs/

Ndivyo binadamu tunavyotakiwa kuishi na kutendeana? Nini thamani ya mtu? Ni mazoea ya ngozi nyeusi kuwa ushenzi, mauaji na mabezo yakifanywa na weupe kuinua pua na ndimi zao hubeua matendo hayo. Lakini bila aibu ngozi hiyo hiyo hukumbatia kwa shangwe na starehe matendo machafu ikiwa midomo imepanuka hadi gego la mwisho laonekana na kukenua meno, ikishangilia maovu yaliofanywa na mweusi! Maskini!

Nilitukanwa kwa nguvu, nikapigwa teke lililochana nguo zangu kwa amri ya Lambo. Nilifanyiwa hivyo kwa sababu sikuwa na cheo? Sikuwa na kazi? Au sikustahili kuheshimiwa kama mtu?

“Nilimhonga fedha kemkem, kwa lazima yake aghalabu, nikaambulia kero, nikaambulia hewa.”

Lambo huko hakujali. Kitendo kilichoniudhi sana ni kule kumlaghai binamu yangu Lulu, kumpa mimba. Alimlaghai pia mchumba wangu, kuwa angempa kazi, kumbe ilikuwa hatua kubwa ya kuniharibia tunda langu. Nini tegemeo la Lambo kutoka kwangu kama sio kisasi? Nitamfuata mke wake. Lakini … Ayavuliaye maji nguo hulazimika kuyaoga.

Kabla sijachukua hatua yoyote ile kuhusu mke wake, lazima nimfuate tena Lambo ili nimpe maoni yangu juu ya suala zima.

Kwanza, nataka kumweleza wazi kuwa tabia yake hailingani na miiko ya viongozi wetu; na wala si mtawala. Amedhaminiwa cheo na vyombo vya umma kwa manufaa ya umma.

Nataka kumkumbusha kuwa si halali yangu wala si wajibu wangu kumwingilia yeye katika shughuli zake za starehe. Aidha, starehe zake zinapoponza haki za watu wengine lazima akumbushwe kujirudi.

Nataka kumkumbusha pia juu ya gari letu. Waangalie wafanyakazi wanavyoteseka wakichapa mguu, shoto – kulia, moja – mbili, kuelekea kiwandani, wakati gari wanalostahili linabebeshwa mijanajike isiyohusika. Hatari kwelikweli, mume wa mtu huyu!

Mbunda Msokile, *Nitakuja kwa siri* (1981)



https://xtremepape.rs/

**2.**

**Adabu**

Mtoto mpembejee, akuwapo umpembe,
Ovu umkemelee, simkumbalie chembe,
Mpaka azowelee, yale mema ajipambe,
Adabu sifa pekee, akiwa nayo kiumbe.

Katu usimchekee, muache vivyo avimbe,
Wala usimlemee, kwenye mapambo mpambe,
Azidi atengenee, wamuanao waambe,
Adabu sifa pekee, akiwa nayo kiumbe.

Kupiga mwana mzee, kwa ajili asiombe,
Hivyo baba usilee, si mwema huo ujumbe,
Wamfanya akolee, atie mpini jembe,
Adabu sifa pekee, akiwa nayo kiumbe.

Mwanao muogelee, kwa maneno umrambe,
Pale azidipo ee, hapo ndipo umchambe,
Muache alie mee, kama mbuzi au ng’ombe,
Adabu sifa pekee, akiwa nayo kiumbe.

Mwana asiye heshima, huchukiza kwa viumbe,
Hata kwa baba na mama, nipulikize nikwambe,
Kuchukiza ni lazima, ingawaje nami nambe,
Adabu sifa pekee, akiwa nayo kiumbe.

Mtoto anapopinda, yakupasa umfimbe,
Japokuwa wampenda, jitahidi umlumbe,
Kwa maneno kumtanda, yenye ukali wa wembe,
Adabu sifa pekee, akiwa nayo kiumbe.

Hayo yote kuyasema, sipendelei viumbe,
Wakulaumu lawama, hayo sitaki waombe,
Ndipo nikafanya hima, rafiki yangu nikwambe,
Adabu sifa pekee, akiwa nayo kiumbe.

M Mzenga na S Hijazy, katika *Nguzo za Ushairi wa Kiswahili* (1989)

https://xtremepape.rs/